# TPSC kinavyowajenga kitaaluma watumishi wa umma katika kuwahudumia wananchi

> TPSC inatoa elimu ikiwa ni mkakati wa kuiunga mkono serikali katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa Tanzania mpya yenye neema kwa raia wake. Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPSC, Dk. Ernest Mabonesho, *anasema chuo hicho kilianzishwa mwaka 2000 chini ya Sheria ya* Wakala Namba 30 ya mwaka 1997 kupitia Mpango wa Uboreshaji Utumishi wa Umma (PSRP) kikitoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

**NA MWANDISHI WETU**

CHUO cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) ni chuo cha serikali ambacho kipo chini ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

TPSC inatoa elimu ikiwa ni mkakati wa kuiunga mkono serikali katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa Tanzania mpya yenye neema kwa raia wake.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPSC, Dk. Ernest Mabonesho, anasema chuo hicho kilianzishwa mwaka 2000 chini ya Sheria ya Wakala Namba 30 ya mwaka 1997 kupitia Mpango wa Uboreshaji Utumishi wa Umma (PSRP) kikitoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

*Anasema mafunzo ya muda mfupi yanatolewa kwa watumishi wa umma kwa lengo la* kuwajengea uwezo, kuongeza ufanisi, kuimarisha utendaji kazi watoe huduma bora kwa umma kuzingatia weledi na matokeo chanya.

Katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Chuo kimeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa umma 7,241.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu huyo anabainisha kati ya watumishi waliopatiwa mafunzo 1,642 walipewa ya awali, 3,965 ya uongozi na utawala na 1,634 ya umahili kwa watumishi wa umma.

"Mafunzo haya yamekuwa chaguo sahihi la kukuza na kuendeleza uwezo wa watumishi wa umma wa kuwahudumia wananchi katika sehemu zao za kazi," anasema.

Mbali na mafunzo hayo, Dk. Mabonesho anasema chuo hicho kimeendesha midahalo kwa njia ya mtandao takriban 423 kupitia kituo cha mafunzo kwa njia ya mtandao (GLS).

Anaendelea kusema kuwa katika kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kuboresha utendaji wa watumishi wa umma, chuo kinatoa kozi kwa kuzingatia mahitaji ya soko.



*Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPSC Dkt. Ernest Mabonesho*

Pia, anasema kinatoa mafunzo yanayowazesha wahitimu kupata ajira na kukidhi mategemeo ya mwajiri ama kujiajiri.

Dk. Mabonesho anasema chuo kimeendelea kutoa ushauri kwa taasisi mbalimbali za serikali namna ya kuboresha utendaji wa taasisi hizo na kufanya tafiti zinazolenga kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma.

"Pia taasisi yetu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu inaendelea kuwajengea watumishi wa umma uwezo waende na kasi ya Rais Dk. Samia ya kuijenga Tanzania yenye neema kwa wote," anasema.

Dk. Mabonesho anaeleza kuwa chuo hicho kinatoa *mafunzo kwa taasisi mbalimbali nchini yenye lengo la kuwajengea uwezo walengwa* kwenda na kasi ya serikali katika ukuaji uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

Anasema anaamini kuwa katika kufanikisha azma hiyo ya serikali, taasisi za umma na idara za serikali hazina budi kuwapeleka watumishi wao chuoni hapo kujengewa uwezo katika masuala anuai yanayohusu utumishi.

"Ni muhimu sana kwa taasisi za umma hapa nchini kuwaleta watumishi wao wapya hapa kwetu kujifunza namna ya uendeshaji wa ofisi, utunzaji kumbukumbu, sheria na utaratibu za utumishi wa umma na namna ya kukabiliana na changamoto za kiutumishi hususan kwa kasi ya mabadiliko ya kiuchumi," anasema.

Dk. Mabonesho anaeleza katika mwaka wa fedha 2022/2023, chuo hicho kupitia sehemu ya mipango na maendeleo kimekamilisha mchakato wa upatikanaji wa viwanja katika mikoa ya Tanga, Mbeya na Dodoma.

Anasema chuo kimeanza awamu ya pili ya ujenzi wa Kampasi ya Singida eneo la Mungu Maji ambapo kukamilika kwa kampasi hiyo kutakipunguzia chuo gharama ya kulipa kodi katika majengo iliyopangwa.

"Hatua hii itawapa fursa watumishi wa umma na wanachuo kutoka Makao Makuu ya Nchi na mikoa jirani kupata mafunzo yanayotolewa na taasisi yetu," anasema.

Anabainisha kwamba tayari chuo hicho kina eneo la muda la kuendeshea mafunzo ambalo liko Mtaa wa Tabora jijini Dodoma na kimefanya ukarabati kiwe kituo mahususi cha kutolea mafunzo kwa watumishi wa umma.

Dk. Mabonesho anabainisha kuwa chuo kimepanuka kwa kuwa na idadi ya wanafunzi, vitendea kazi na idadi ya kozi zimeboreshwa kwa uwiano mzuri.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa chuo hicho anazitaja kozi *zinazotolewa katika chuo hicho ni Utunzaji Kumbukumbu, Nyaraka na Taarifa na Uhazili.*

*Nyingine ni Rasilimali watu, Utawala wa Umma, Ununuzi na Ugavi na Utawala wa Serikali za Mitaa.*

Anasema hivi sasa chuo kinatoa mafunzo katika ngazi ya Shahada ya kwanza kuanzia Septemba, 2017 katika fani za Uhazili na Menejimenti ya Kumbukumbu, Nyaraka na Taarifa katika Tawi la Dar es Salaam.

"Tunawakaribisha watumishi wa umma, wananchi na kwa wenye sifa za kujiunga na Astashahada, Stashahada na Shahada katika kozi mbalimbali kuomba kujiunga. Maombi yanapokelewa kwa njia ya mtandao kupitia tuvuti ya chuo," anaeleza.

Anasema chuo hicho kina matawi sita ambayo ni Dar es Salaam, Tabora Mtwara Tanga, Singida na Mbeya.

Mtaalamu wa masuala ya Utumishi na Ajira, Magesa Bwire ambaye ni mkazi wa Dar es Salaam, anakipongeza chuo hicho kwa kuendesha mafunzo kwa watumishi ambayo ni muhimu katika dunia ya sasa yenye kutawaliwa na utandawazi.

"Ni muhimu sana kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kuwa yanawafanya waende na wakati, hivyo kutoa huduma bora kwa wananchi," anasema.

CamScanner